

Msaada wa Kijamii:

Huduma za Haki za Familia:

Kutoa msaada kwa familia zilizo na utunzaji wa mtoto, ziara kwa mtoto wako, na msaada wa watoto nje ya korti.

Huduma ya bure, ushauri, elimu.

<https://court.nl.ca/supreme/family/fjs.html>

St John's: 729-1183

Residential Tenancies Board:

Ikiwa una maswali au malalamiko yoyote juu ya kukodisha, haki zako au haki za mwenye nyumba yako.

Simu: 729-2608

Nambari ya bure katika Newfoundland and Labrador: 1-877-829-2608
landlordtenant@gov.nl.ca

Labour Standards Division

Hutoa habari na maelezo kuhusu haki na majukumu kazini.

Pia hufanya uchunguzi ikiwa unahisi haki zako zimekiukwa.

Simu: 729-2742

Bila malipo: 1-877-563-1063
LabourStandards@gov.nl.ca

Newfoundland and Labrador Human Rights Commission

Hutoa habari na hufanya uchunguzi wa ubaguzi na unyanyasaji.

Simu: 729-2709

Bila malipo: 1-800-563-5808
humanrights@gov.nl.ca

Uhamiaji, Wakimbizi na Uraia wa Canada

Ikiwa una maswali au tatizo kuhusu hali yako ya uhamiaji.

1-888-242-2100

Office of Immigration & Multiculturalism

1-709-729-7140

immigration@gov.nl.ca

Simu ya Habari ya Kisheria:

Jumatatu hadi Ijumaa
Saa 2: 30 asubuhi hadi 7:30 mchana

Jumatano jioni
Saa 12 jioni hadi saa 3 usiku

Huduma ya Mtandao wa Mawakili:
Jumatatu hadi Ijumaa
Saa 2: 30 asubuhi hadi 7:30 mchana

Jumatano jioni
Saa 12 jioni hadi saa 3 usiku
Dakika 30 za ushauri wa kisheria
ukitolewa na wakili kwa ada ya \$40

Kuna wanasheria walio na
uzoefu wa sheria ya uhamiaji



Simu: (709) 722-2643
Bila malipo: 1-888-660-7788
Barua pepe: info@publiclegalinfo.com

Habari ya Kisheria

Mwongozo kwa wageni



Haki na Jukumu lako wakati wa Kukodisha Nyumba au Fleti:

Mpangaji:

- Lipa kodi kwa wakati.
- Weka nyumba kwa hali safi na urekebishe uharibifu wowote unaoufanya.
- Usibadilisha kufuli, kukata vifaa vya joto, maji au umeme.
- Mjulisha mwenye nyumba yako kwa maandishi ikiwa unataka kuhama.
- Wakati unaweza kuhama inategemea na makubaliano yenu ya kukodisha.
- Fuata sheria na uweke amani.

Mwenye nyumba:

- Hawezi kuingia ndani ya fleti au nyumba yako bila taarifa isipokuwa wakati wa dharura.
- Mwenye Nyumba lazima akupe ilani ya masaa 24 (kwa maandishi) ili kuingia ndani ya nyumba yako.
- Mwenye Nyumba hawawezi kuongeza kodi bila kukupa ilani.
- Kodi haiwezi kuongezewa wakati wa mkataba wa muda maalumu.
- Mwenye Nyumba hawezi kukatisha huduma ya joto, maji au umeme.
- Amana ya usalama inaweza kurudishwa ndani ya siku 10 baada ya mkataba ya kukodisha kumalizika.
- Anaweza kukutoza ada ikiwa kodi yako imechelewa.
- Anaweza kukufukuza ikiwa utashindwa kulipa kodi baada ya siku 3 (malipo ya kila wiki) au siku 5 (malipo ya kila mwezi au muda maalumu).

* Una haki ya kuwa na msaidizi au mtafsiri ili kukagua makubaliano yako ya kukodisha na kuwa na wewe wakati unatia saini.

Haki zako Kazini:

Ikiwa una haki ya kufanya kazi nchini Canada, unalindwa na sheria.

- Mshahara wa chini ni \$11.40 kwa saa
- Mshahara wa chini wa saa za ziada ni \$17.10 kwa saa
- Wiki ya kawaida ya kazi ni masaa 40 kwa wiki.
- Mapunguzo yoyote kutoka kwa mshahara wako kwa makazi lazima yaorodheshwa katika mkataba wako.
- Ni haki yako kuchukua ruhusa ya likizo ya ugonjwa au ya familia Uja uzito Ili kumlea mtoto wako Kifo katika Familia Kutunza jamaa anayekufa Vurugu ya Familia
- Ubaguzi na udhalilishaji hauruhusiwi kazini.
- Dhulma ya kimapenzi hairuhusiwi kazini.
- Ni haki yako kuripoti ubaguzi na udhalilishaji
- Wanafunzi wa Kimataifa wanaweza kufanya kazi hadi Masaa 20 kwa wiki wakati wa kipindi cha masomo na hadi masaa 40 kwa wiki wakati wa mapumziko -ikiwa wanatimiza masharti.

Usalama

- Unaweza kukataa kazi isiyo na usalama.
- Una haki ya mafunzo ya kazi.
- Una haki ya kufanya kazi pasipo na unyanyasaji na ubaguzi.

Haki zako kama Familia

Sheria za familia ni pamoja na:

- Talaka au kujitenga
- Haki ya utunzaji wa mtoto au watoto wako
- Kumfikia mtoto au watoto wako
- Msaada wa kifedha kutoka kwa mzazi mwingine

Vurugu ni uhalifu nchini Canada. Ikiwa utapatikana na hatia unaweza kufungwa gereza au kupokea mashtaka ya jinai. Vurugu za familia ni pamoja na:

- Kumpiga ngumi, kumchapa, kumpiga mateke mke wako, mume, mwenzi au mtoto, kumzuia na kumfungia, kutumia vitisho na utumiaji wa silaha.
- Kutompaa ruhusa mwenzi wako afanye kazi, awe na fedha, awe na marafiki, kufurahiya utamaduni wake, kuzuia huduma ya matibabu, au kumtenga.
- Mwingiliano wa kimapenzi usiofaa. Ni kinyume cha sheria kuwa na mawasiliano yoyote ya kimapenzi na mtu ikiwa hataki, **hata ikiwa mmeoana au mna uhusiano.**
- Mtoto anaweza kuondolewa nyumbani ikiwa yuko katika hatari ya kudhuriwa.
- **Ikiwa unakabiliwa na vurugu ya kifamilia, unaweza kuvunja mkataba wako wa kukodisha.**

Fanya ombi kwa Mkurugenzi wa Residential Tenancies

Ni lazima utoe ilani ya siku 30

Una haki ya kuuliza mtafsiri.

Una haki ya kuongea na wakili.

Unaweza kumleta msaidizi wako wakati wowote wa miadi ya kisheria.

Wakili anaweza kuidhinisha hati za zilizotafsiriwa.